

# TAARIFA KWA WAZAZI



## KAMA FAMILIA YAKO INAISHI KATIKA HALI YOYOTE KATI YA ZIFUATAZO:

Katika makazi ya muda

♦  
Katika hoteli au kambi kutokana na kukosekana kwa malazi mazuri mbadala

♦  
Katika gari, hifadhi, jengo lililoachwa bila kutumika, au kituo cha basi au garimoshi

♦  
Wanaishi na watu wengine kutokana na kupoteza makazi au ugumu wa uchumi

*Watoto wako wenyewe umri wa kwenda shuleni wanaweza kuwa na haki  
fulani naulinzi chini ya Sheria ya shirikisho ya McKinney-Vento.*

### Watoto wako stahiki wana haki ya:

- Kupokea elimu ya umma inayofaa bila malipo.
- Kusajiliwa shuleni haraka, hata kama kunakosekana hati ambazo kwa kawaida huwa zinahitajika kwa ajili ya usajili.
- Kusajiliwa shuleni na kuhuduria masomo wakati shule inakusanya hati zinazohitajika.
- Kusajiliwa kwenye shule za ndani; au kuendelea kuhuduria shule zao za awali (shule walizohuduria walipokuwa na makazi ya kudumu au shule ambayo alisajiliwa mara ya mwisho), kama hilyo ndilyo chaguo lako na inawezekana.
  - \* Kama shule ya wilaya inaanini kwamba shule ulioichagua haina maslahi mazuri kwa watoto wako, basi wilaya lazima ikupe maelezo kwa maandishi kuhusu nafasi yake na wakujulishe haki yako ya kukata rufaa kuhusu maamuzi yao.
- Kupokea usafiri kwenda na kutoka shule ya awali, kama utaomba hii.
- Kupokea huduma za elimu sawa na zile zinazotolewa kwa wanafunzi wengine, kulingana na mahitaji ya watoto wako.

*Kama unaamini watoto wako wanaweza kuwa stahiki, wasiliana na mtu wa uhusiano wa ndani kujua huduma na misaada gani inaweza kupatikana. Kunaweza kuwa pia na msaada kwa watoto ambao hawajaanza shule.*



Uhusiano wa ndani

Mratibu wa Jimbo

Kama unahitaji usaidizi zaidi na mahitaji ya elimu kwa watoto wako,  
wasiliana na Kituo cha Taifa kwa ajili ya Elimu kwa Wasio na Makazi:

1-800-308-2145 • [homeless@serve.org](mailto:homeless@serve.org) • [www.serve.org/nche](http://www.serve.org/nche)